


Agizo la Kukaa Nyumbani-Jimbo la Ontario

KUANZIA Tarehe 8 Mwezi wa nne 2021

Usahihi wa maelezo: Aprili 7, 2021



Mikusanyiko na Kuwa Karibu na Watu

- Usikusanyike ndani na mtu yeyote wa nje ya nyumba yako
- Usimtembelee mtu yeyote wala usiruhusu wageni nyumbani kwako
- Kama unaishi peke yako, unaweza kukutana na wakazi wa nyumba nyingine moja tu
- Mikusanyiko ya nje isizidi watu watano (5)
- Kikomo cha asilimia kumi na tano (15%) kwa mikutano ya ndani na hakuna kikomo kwa mikusanyiko ya nje kama ibada za dini, harusi au mazishi tu.

Shule na sehemu za Kulea Watoto

- Shule zimefunguliwa isipokuwa miji ya Toronto na Peel. Miji hii imefungwa mpaka baada ya likizo ya kipindi cha Masika
- Sehemu za kulea watoto zimefunguliwa

Kodi na Kufukuzwa kwenye nyumba

Wapangaji wasifukuzwe katika kipindi chote cha agizo la kukaa nyumbani.

Nini Kipo wazi?

- Huduma za baa na migahawa (kuchukulia nje au kuletewa nyumbani)
- Maduka ya rejareja yamefunguliwa kwaajili ya huduma za chakula, afya, vifaa vya usafi, vifaa vya wanyama wa ndani, na matunzo binafsi.
- Maduka makubwa, vituo vya bustani, maduka ya dawa, huduma za meno, macho, maduka ya vifaa vya ujenzi na ulinzi, maduka yanayouza, kukodisha au kutengeneza vifaa vya matibabu, simu, magari na vifaa vingine yamefunguliwa kuanzia saa moja asubuhi hadi saa mbili usiku **kwa kuweka miadi**. Kikomo cha idadi ya watu ndani ni 25%. Huduma za kuletewa vitu majumbani ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa tatu usiku.
- Biashara zisizo muhimu zimefunguliwa kwaajili ya kuchukua vitu nje ya duka kuanzia saa moja asubuhi hadi saa mbili usiku **kwa miadi**. Kuletewa nyumbani ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka saa tatu usiku.
- Maduka makubwa yamefunguliwa kwaajili ya kuchukua vitu kwa haraka na huduma nyeti kama maduka ya dawa na madaktari wa meno)
- Sehemu za nje za michezo kama viwanja vya gofu na mpira wa kikapu



Chanzo: Wizara ya Afya, Ontario
<https://covid-19.ontario.ca/zones-and-restrictions>

{ REFUGEE } 613
{ RÉFUGIÉ } 613

Nini Kimefungwa?

- Sehemu za kufanya mazoezi na huduma binafsi kama za kutengeneza kucha na saluni nywele
- Makasino, kumbi za bingo, michezo ya kubahatisha na kumbi za sinema.
- Kula ndani ya migahawa au sehemu zinazouza chakula

Tunaweza kufanya nini?

- Fanyia kazi nyumani kama inawezekana
- Toka nje kwa sababu za msingi kama kazi, shule, kununua vyakula, dawa, huduma za afya na kusaidia wahitaji.
- Fanya matembezi, endesha baiskeli au fanya mazoezi ya viungo
- Vaa barakoa na kaa mita mbili mbali na watu!
- Kaa ndani ya mtaa wako na epuka safari zisizo za lazima-hata ndani ya mkoa wako

